# Siku 10 za Mwaka wa 2023: Kujitayarisha kwa Mavuno

*“Baada ya hayo nikaona, na tazama, mkutano mkubwa sana ambao hapana mtu awezaye kuuhesabu, watu wa kila taifa, na kabila zote na jamaa na lugha, wamesimama mbele ya kile kiti cha enzi, na mbele ya Mwana-Kondoo, wamevaa mavazi meupe, na matawi ya mitende mikononi mwao. , 10 wakilia kwa sauti kuu, wakisema, Wokovu una Mungu wetu aketiye juu ya kiti cha enzi, na Mwana-Kondoo. Ufunuo 7:9-10*

“Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi…” Mt 28:18-20

**Tunapo taja “Siku 10” ni sehemu ya Mpango wa Mungu kwa ajili ya Uamusho na Umoja wa Kanisa, Kuokoa waliopotea, na hatimaye, kuandaa njia kwa ajili ya Kurudi Kwake Yesu Kristo mara ya pili.** "Siku 10 za Kushangaza" ni utaratibu unao tia mizizi yake katika siku Kumi za utaratibu wa kiblia sawa jinsi siku hizi zinazo tajwa katikati ya **Sikukuu za Baragumu** (Rosh Hashanah) na **Siku ya Upatanisho** (Yom Kippur). Sikukuu hizi zinaonyesha kiunabii Kurudi kwa Yesu mara ya pili. Mungu iko katika kuwaleta waje kwake umati mkubwa wa watu kutoka katika kila taifa, kabila, jamaa na lugha. Jukumu yetu sisi ni kushirikiana Naye Bwana kusudi ya kuona Ufalme Wake ukiinuliwa juu na kupanuka mupaka pale wanadamu wote wanapo pata kufikia kusikia habari kuhusu utukufu wa Mungu.

**Tunaalikwa kuchukua jukumu la kutangaza Habari Njema ya Wokovu, lakini kazi hii lazima ianzie kwa hatua ya maombi**. Sisi kama wana na binti za Mungu Aliye Juu Sana, tunapojazwa na upendo wa Mungu, mara nyingi tunajisikia mioyo yetu ikichochomea ili kutangazia watu wengine ujumbe huo wa upendo Wake Yeye Mungu.

Mungu hutenda kazi ni kwa njia ya maombi yanayo ombwa kwa  imani, kuutoka vinywa vya watoto wake ambao wanasukumwa na jinsi wanavyo waonea wengine huruma na wanao jitolea kujibu wito wa kuitikia Sauti ya Mungu kwa utiifu. Katika hii miaka michache iliyopita, kazi ya maombi na kazi ya kupeleka Habari Njema kwa walio mbali zimeanza kuungana pamoja kusudi ya kutiana nguvu.

Mupaka sasa hivi, baada ya mika 2000 iliyokwisha pita, Kazi bado ingali inatungoja ya Agizo Kubwa alilo tuachia Yesu :

- Asilimia 80 ya Waislamu duniani bado hawajui hata Mkristo mmoja.
- Makabila 1,708 ya Makundi ya watu hawajakuwa bado na Biblia katika lugha yao wenyewe.
- Kuna Makabila 5,000 ya Makundi  ya watu ambayo kwa jumla inayo watu bilioni 2.6 na ambako kati yao ukukutana na watu  1,000 utakuta kati ya hawa watu 1,0000 kuko Mufuasi wa Yesu chini ya mumoja (1).
- Ikiwa tutaendelea kutumika Kazi ya Mungu jinsi tuko natumika leo, maana yake, watu wa kabila ya Wachina milioni 500 watakufa bila kamwe kusikia habari za Yesu hata kidogo.

**Muungano Wetu Huu wa Maombi ya Siku 10** hufanya kazi ya kuunganisha  huduma nyingi ulimwenguni kusudi ya ku ungana katika maombi na katika kazi ya kueneza injili kwa pamoja. Siku hizi za majuzi juzi, kulianzishwa Mpango mpya unao itwa Ombeni 110 (www.110cities.com), ulio anzishwa kutokana na habari ya maisha ya waamini walio julikana kwa jina la wa Wamoravia walio ishi miaka 300 iliyopita. Lengo la mupango huu lilitokana na utafiti ulio fanyika na Umoja wa dunia nzima wa Makanisa ya nyumbani ambao ulionyesha wazi kwamba kuko miji hii 110 ambayo imeiva kwa ajili ya mavuno. Zaidi ya hayo, karibu vikundi vyote vya watu ambao hawajafikiwa bado na injili duniani vinavyo watu walio na mahusiano nao katika miji hii  110! Viongozi hawa wa Makanisa ya Manyumbani pia walieleza kuwa wanayo timu lililo tayari kusudi ya kuzindua Kazi ya Pamoja ya upandaji wa Makanisa na kufanya watu kuwa wanafunzi wa Yesu Kristo katika miji hii wakakti huu tunapo karibia kufikia mwaka wa 2025.

**Kwa kuwa tunayo Imani kuwa Mungu atasimamisha kila kitu kwenye miji kwa Siku 10 katika toba, maombi, kufunga, na kuabudu ili kuomba na kukizunguka kiti cha enzi, mchana na usiku, na huku waamini toka kote ulimwenguni- pia tunaomba kutokeye mabadiliko na uamsho katika**

**miji hii 110 inayo patikana kwenye mataifa mbali-mbali ulimwenguni.** Nia na Moyo wa Mungu ni kwamba mtu yeyote asiangamie bali wote wafikie toba. Yesu anatualika kugeuka kutoka kwa Ufalme wa Ulimwengu huu na kugeukia Ufalme Wake wa haki, amani na furaha katika Roho Mtakatifu. Roho na Bibi-arusi husema, “Njoo.”
Mupango wa Siku 10 unaalika kila Kusanyiko la Waamini kuchukua mojawapo ya miji hii 110 na kuelekeza maombi yanayo lenga muji huo. Tunapokusanyika ili kuomba, kutubu na kugeuza mioyo na nia zetu kutoka kwa njia ya ulimwengu huu na kuelekea njia ya Mungu, pia tutaombea jiji letu tunapopatikana kusudi na muji wetu pia upate kupitia mabadiliko sawa sawa na muji tunao uombea.

Kila siku, tutaomba tukifuata kichwa cha Neno linalo patina na nia ya ***kugeuka kutoka kwa mambo ya ulimwengu na kuelekea kwa Mfalme Wetu Yesu na Ufalme Wake.*** Tutaelekeza mawazo kwenye eneo moja la dunia, na kukumbuka ni muji gani kati hii miji 110 unao patikana katika lile eneo la Ulimwengu (bila kusahau miji mingine yenye inapatikan katika lile eneo), na kuwa na maombi kwa ajili ya waamini, kwa ajili ya kanisa mwili wa Kristo, na kwa ajili ya waliopotea. Siku ya 9 na ya 10 itaelekea miji inayo hitaji kushugulukiwa kiupekee na iliyoko katika bara la Amerika na Karibea ambayo ni nyumbani kwa vikundi vya watu wa diaspora na pia inatuma vituo kwa wamishonari. Unapoomba katika kila sehemu, usijiombee wewe mwenyewe tu, bali pia uombe kwa ajili ya watu unao ishi nao, pia kwa ajili ya jimbo lako na pia kwa ajili ya taifa lako, na kwa ajili ya miji hii na maeneo yao pia kwamba wao pia wageuke kutoka gizani na kuingia kwenye nuru, wakati Juwa la Nuru ya Injili itakapo waangazia. Wakati unapo omba uzingatiye sana mji wako ulio uchagua ku uombea kusudi yak u uleta mbele ya Kiti cha Enzi katika maombi yako ya kila siku.

**Omba kwamba Mungu asukume mbele zaidi Watenda kazi kwa wingi wakutosha katika mashamba yaliyoiva kwa ajili ya mavuno yaliyo tayari ulimwenguni kwa ajili ya Utukufu Wake!**

## Vichwa Vya Neno Kwa Siku 10 Za Kuomba na Kufunga

| GEUKA KUTOKA: | | GEUKIA UPANDE WA: |
|---|---|---|
| **Siku 1:Giza** | → | **Nuru** |
| **Siku 2: Kutokujali** | → | **Kukimbilia Walio gizani** |
| **Siku 3: Matengano** | → | **Umoja wa Kanisa** |
| **Siku 4: Kulaumiana** | → | **Upendo** |
| **Siku 5: Ukimia** | → | **Kutumikiana** |
| **Siku 6: Uchunguzi** | → | **Kujitoa kabisa** |
| **Siku 7: Kuogopa watu** | → | **Woga wa Mungu** |
| **Siku 8: Pupa** | → | **Kutumikiana** |
| **Siku 9: Tumikia v ya dunia** | → | **Kuishi kwa ajili ya Ufalme** |
| **Siku 10: Kuangalia nyuma** | → | **Kutazama Juu** |

# SIKU YA 1:

# KUTOKA NDANI YA GIZA NA KUINGIA KWENYE NURU

**TITO 2:11-14** *Kwa maana neema ya Mungu iwaokoayo watu wote imefunuliwa, nayo yatufundisha kukataa ubaya na tamaa za kidunia, na kuishi na kiasi kwa haki na utauwa katika ulimwengu huu wa sasa, tukitazamia tumaini, na kufynuliwa kwa utukufu wa Mungu mkuu na Mwokozi wetu Yesu Kristo, ambaye alijitoa mwenyewe kwa ajili yetu ili atukomboe na maasi yote na kujisafishia watu kwa ajili yake mwenyewe ambao wana bidii kwa ajili ya matendo mema."*

**KUABUDU: Wewe ni BABA YETU ULIYE MBINGUNI, JINA LAKO NI TAKATIFU**[1]

> **1 SAMUELI 2:2** "H*akuna aliye mtakatifu kama BWANA; hakuna mwingine ila wewe; hakuna Mwamba kama Mungu wetu."*
>
> **KUTOKA 15:11** "*Ee Bwana, ni nani kati ya miungu kama wewe? Ni nani aliye kama wewe, mwenye utukufu katika utakatifu, mwenye kustaajabisha kwa mambo ya utukufu, mwenye kufanya mambo ya ajabu?"*

**KUTUBU :** *Utusamehe Bwana kwa kuwa tumechagua njia yetu wenyewe pahali pa kujinyenyekeza chini ya uongozi wako wenye hekima wenye upendo na mwongozo. Utusamehe dhambi zetu, Ee Mungu:*


- *Tamaa ya mwili*
- *Tamaa ya macho*
- *Kiburi*

**1 JOHANA 2:15-17** "*Msiipende dunia, wala chochote kilicho katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia. Ulimwengu na tamaa zake unapita, bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu anaishi milele."*

**KWA SAUTI KUBWA UWAALIKE WATU KUINGIA MAVUNONI HUKO: *JAKARTA, INDONESHIA***

***Mingini ingine katika hiyo eneo:***

- Phnom Penh, Cambodia
- Vientiane, Laos
- Yangon, Myanmar
- Bangkok, Thailand
- Ho Chi Minh, Vietnam
- Hanoi, Vietnam
- Kuala Lumpur, Malaysia
- Bandung, Indonesia
- Makassar, Indonesia
- Medan, Indonesia
- Banjarmasin, Indonesia
- Surabaya, Indonesia




<u>**ENEO MOJA KATI YA MIJI 10**</u> **:** ***ENEO LA PACIFIKI YA KUSINI / AZIA YA KUSINI YA MASHARIKI***

*ENEO LOTE LINA :Watu milioni 723*

*Hesabu ya Makabila yasiyo wahi kuwa na hata Kanisa moja kwenye miji yao ni ni Makabila 755*

*Hesabu ya Makabila ya watu ambao bado hawaja fikiwa hata kidogo na injili ni Makabila 33*

**ZABURI 67:1-2** *"Mungu na atufadhili, na kutubariki, na kutuangazia uso wake, njia zako zijulikane duniani, wokovu wako katika mataifa yote."*

1. Omba Mungu awakomboe waliofungwa gizani waingie katika nuru yake.
2. Ombea ushirika wa kuzidisha ili kupata ufunuo ulioenea wa utukufu wa Bwana. Hab. 2:14
3. Ombea tafsiri za Biblia katika lugha hizi muhimu kwa eneo hili: : West Albay Bikol, Brunei, & Phuan..

**UGEUZE GIZA KUWA NURU MIONGONI MWA JIRANI ZAKO**

Fanya hatua leo hii ya Kutembea mahali unapoishi pamoja na Kuomba. Kama ukikutana na jirani mumoja, anzisha mazungumuzo naye na muulize hivi, "Je kuko kitu moja fulani ambacho ninaweza kukuombea kukihusu?"

**1 PETRO 2:9-10** *"Bali ninyi ni Uzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wake maalum, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu; 10 ambao hapo kwanza mlikuwa si taifa, bali sasa ni watu wa Mungu, ambao hamkupata rehema, bali sasa mmepata rehema."*

# SIKU YA 2: GEUKA KUTOKA HALI YA KUTOKUJALI ILI KUFIKIA KU WAKIMBILIA WALIO DHAMBINI

**1 YOHANA 3:17-18** ***"L****akini mtu akiwa na riziki ya dunia, akamwona ndugu yake ni mhitaji, akamzuilia moyo wake, upendo wa Mungu wakaaje ndani yake? Watoto wadogo, tusipende kwa neno wala kwa usemi, bali kwa tendo na kweli."*

**KUABUDU (KUGEUZA NIA): Wewe ni EMMANUEL, MUNGU PAMOJA NASI**[2]

**MATAYO 1:23** *"Tazama, bikira atachukua mimba, naye atamzaa mwana, nao watamwita jina lake Imanueli, yaani, Mungu pamoja nasi."*

**WARUMI 5:8** *"Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.."*

**KUTUBU (KUGEUZA NIA) :** *Utusamehe kwa kushindwa kukuiga wewe Yesu, ambaye hukubaki kubaki katika utukufu na faraja yako, bali ulichukua hatua hata tulipokuwa adui zako, ili utuokoe. Utusamehe kwa kuthamini faraja na urahisi badala ya kuchukua hatua ya kushiriki habari zako njema na wengine hata kama itatubidi sis kuteseka katika kuifanya. Utusamehe dhambi zetu, Ee Mungu;*

- *Kiburi*
- *Upuuzi*
- *Kutojali*

**EZEKIELI 16:49-50** *"Basi dhambi ya Ndugu yako mke Sodoma ilikuwa hii: Yeye na binti zake walikuwa na kiburi, walishiba, wala hawakujali; hawakuwasaidia maskini na wahitaji. Walijivuna na kufanya machukizo mbele yangu. Kwa hiyo niliwaangamiza kama ulivyoona."*

**KWA SAUTI KUBWA UWAALIKE WATU KUINGIA MAVUNONI HUKO : BEIJING, UCHINA**

***Miji ingine ya eneo hili:***

- Pyongyang, Korea Kaskazini
- Ulaanbaatar, Mongolia
- Beijing, China
- Guangzhou, China
- Kunming, China
- Xining, China
- Chengdu, China
- Hohhot, China
- Wuhan, China
- Nanning, China

ENEO MOJA KATI YA MIJI 10 : *KASKAZINI YA KANDONI MWA ASIA*

*ENEO LOTE NZIMA : Lina Wakaaji bilioni 1.639*

*525 ndiyo hesabu ya Makabila ambayo bado hawana Kanisa hata moja kwenye miji yao*

*305 Ndiyo hesabu ya makabila ambayo kamwe hawaja fikiwa hata kidogo na Injili*

**MATAYO 5:14-16** *"Ninyi ni nuru ya ulimwengu. Mji uliojengwa juu ya mlima hauwezi kufichwa. Wala watu hawawashi taa na kuiweka chini ya bakuli. Badala yake huiweka juu ya kinara chake, nayo yatoa nuru kwa wote waliomo ndani ya nyumba."*




1. Ombea waamini walazimishwe na upendo wa Mungu kuwafikia waliopotea.
2. Ombea kanisa la chinichini liwe na uamuzi usio tikiswa na lolote katika kazi ya kutangaza wokovu wa Yesu.
3. Ombea tafsiri za Biblia katika lugha hizi muhimu kwa eneo hili:Lugha ya Alama za Vidole ya Kichina, Jinyu ya Kichina, na Min Zhong ya Kichina.

**GEUKA TOKA KUTOKUJALI FIKIA KUWA NA NIA KUBWA:**
Simama na uende kwenye restorent ya kiasilia, kwenye duka ao karibu na unako ishi. Tembea pamoja na kuomba huku ukijitahidi kuzungumuzia mutu kuhusu upendo na uzima miongoni mwa watu wa hii utamaduni.

**MATAYO 28:18-20** *"Kisha Yesu akaja kwao, akasema nao, akasema, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Kwa hiyo, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi. Na hakika mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari."*

# SIKU YA 3: KUGEUKA KUTOKA MATENGANO NA KUUFKIA USHIRIKA WA PAMOJA

**WAEFESO 4:1-6** *"...Nawasihi kuishi maisha yanayoustahili wito mlioitiwa. Iweni wanyenyekevu na wapole kabisa; muwe na subira, mkichukuliana katika upendo. Jitahidini kuuhifadhi umoja wa Roho kwa njia ya kifungo cha amani. Kuna mwili mmoja na Roho mmoja, kama vile mlivyoitiwa tumaini moja mlipoitwa; Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja; Mungu mmoja na Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote."*

**KUABUDU : Wewe ni MUNGU MMOJA katika NAFSI TATU, Umoja katika utofauti[3]**

> **1 PETRO 1:1-2** *"Kwa wateule wa Mungu, … ambao mlioteuliwa kwa kadri ya mpango wa Mungu Baba alioufanya muda mrefu uliopita, muwe wake kwa kufanywa watakatifu na Roho Mtakatifu …kwa kunyunyiziwa damu ya Yesu Kristo"*

**LUKA 3:22 :** "*Roho Mtakatifu akashuka juu yake [Yesu] mwenye umbo kama hua, na sauti ikatoka mbinguni ikasema : Wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu, ninaye pendezwa nawe.."*

**KUTUBU (KUGEUZA NIA):** *Utusamehe kwa kujifikiria zaidi sisi wenyewe kuliko wengine, kwa kujali zaidi kujitengenezea jina badala ya kumwinua Yesu na kutumikiana kwa upendo. Utusamehe dhambi zetu, Ee Mungu:*

- *Ubinafsi na Kujitegemea*
- *Kuinua kikundi changu juu ya wengine*

- *Kushindwa kujitiisha na kuwatumikia wengine katika Bwana*

**1 KORINTO 12:24-27** *; "Lakini jinsi hii Mungu ameuunda mwili, akivipa heshima zaidi kiungo kilichopungukiwa, ili pasiwe na mafarakano katika mwili, bali viungo vitunzane. kiungo kimoja kikiumia, viungo vyote huumia pamoja; kiungo kimoja kikitukuzwa, vyote hufurahi pamoja. Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na kila kimoja cha viungo ni sehemu ya mili huu"*

**KWA SAUTI KUBWA UWAALIKE WATU KUINGIA MAVUNONI HUKO : Mumbai, India**
**Ni ENEO Moja Kati ya Miji 10 ya Huko : *AZIA YA KUSINI***




*ENEO LOTE NZIMA : Lina Wakaaji bilioni 1.869*
*Hesabu ya Makabila ambayo bado hawana Kanisa hata moja kwenye miji yao : Makabila 3,661*
*Hesabu ya Makabila ambayo kamwe hawaja fikiwa hata kidogo na Injili ni : 3,148*

**ZABURI 22:27** *"Miisho yote ya dunia itakumbuka na kumgeukia Bwana, Na jamaa zote za mataifa watasujudu mbele zako."*

1. Ombea waamini wafanye kazi pamoja vizuri wote wakiwa kama viungo vya Mwili wa Kristo.
2. Mwombe Mungu avunje kuta zinazogawanyika kati ya Mashirika mbalimbali ya Waamini na kuzidisha ushirika. :
3. Ombea tafsiri za Biblia katika lugha hizi muhimu kwa eneo : Kachari, Khah, and Spiti Bhoti.

***Miji ingine ya Eneo hii :***

- Kathmandu, Nepal
- Chittagong & Dhaka, Bangladesh
- In India: Ahmadabad, Amritsar, Asansol, Bangalore, Bhopal, Delhi, Hyderabad, Jaipur, Kanpur, Kolkata, Lucknow, Mumbai, Patna, Prayagraj, Siliguri, Srinagar, Surat & Varanasi

**GEUKA KUTOKA KUJIWEKA KANDO UELEKEYE UMOJA :** Piga simu na ualike rafiki mpya, mwanafamilia, au mtu unayemfahamu ajiunge nawe kwa mkusanyiko wako unaofuata wa maombi.

**WAGALATIA 3:28** *"Hakuna Myahudi wala Myunani, mtumwa wala mtu huru, hakuna mwanamume na mwanamke; kwa maana ninyi nyote mmekuwa mmoja katika Kristo Yesu."*

# SIKU YA 4: KUTOKA KATIKA UBAGUZI KUFIKIA HALI YA UPENDO WA NDUGU

**1 JOHANA 4:20-21** *"Mtu akisema, Nampenda Mungu, lakini anamchukia ndugu yake, ni mwongo. Kwa maana mtu yeyote asiyempenda ndugu yake ambaye amemwona, hawezi kumpenda Mungu ambaye hajamwona. Naye ametupa amri hii: Yeyote anayempenda Mungu lazima ampende pia ndugu yake."*

**KUABUDU : Nyinyi ni MAWAKILI na AWAPATANISHI[4]**

**2 WAKORINTO 5:18-20** *"Haya yote yatokana na Mungu, ambaye kwa Kristo alitupatanisha sisi na nafsi yake, akatupa huduma ya upatanisho; yaani, katika Kristo Mungu alikuwa akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake, asiwahesabie makosa yao, naye akiweka kwetu ujumbe wa upatanisho."*

**WAEFESO 2:14-17 "***Kwa maana yeye ndiye amani yetu, aliyetufanya sisi sote wawili kuwa wamoja, akaubomoa katika mwili wake ukuta uliogawanya wa uadui, kwa kuibatilisha sheria ya amri zilizowekwa katika maagizo, ili apate kuumba ndani yake mtu mmoja mpya. mwanadamu badala ya hao wawili, akiisha kufanya amani, na kutupatanisha sisi sote na Mungu katika mwili mmoja, kwa njia ya msalaba, akiua ule uadui."*

**KUTUBU (KUGEUZA NIA):** *Utusamehe kwa kuweka chuki na kutosamehe katika mioyo yetu wakati umetusamehe mengi! Utusamehe dhambi zetu, Ee Mungu:*

- *Ubaguzi na chuki*
- *Uchungu na kutosamehe*
- *Kushindwa kuwapenda wengine kama ulivyotupenda sisi*

**WARUMI 12:17-21** *" Msimlipe mtu ovu kwa ovu. Iweni waangalifu kufanya yaliyo sawa machoni pa kila mtu. Ikiwezekana, kwa kadiri inavyowategemea ninyi, kaeni kwa amani na watu wote..."*

**KWA SAUTI KUBWA UWAALIKE WATU KUINGIA MAVUNONI HUKO : Tashkent, Uzbekistan**
Ni ENEO Moja Kati ya Miji 10: ***ASIA YA KATI***

*ENEO LOTE NZIMA : Lina Wakaaji milioni 304.5*
*Hesabu ya Makabila ambayo bado hawana Kanisa hata moja kwenye miji yao : Makabila 398*
*Hesabu ya Makabila ambayo kamwe hawaja fikiwa hata kidogo na Injili ni : Makabila 398*




**WAKOLOSAI 1:21-22** *""Hapo zamani mlikuwa mmefarakana na Mungu, na mlikuwa adui katika nia zenu kwa sababu ya mwenendo wenu mbaya. Lakini sasa amewapatanisha ninyi kwa mwili wa Kristo kwa njia ya mauti, ili awalete ninyi watakatifu mbele zake, bila mawaa wala lawama."*

1. Mwombe Mungu aondoe ubaguzi wa kitamaduni au kidini katikakti ya waamini.
2. Ombea Mwili wa Kristo uushinde ubaguzi kwa njia ya kuwapenda adui zao.
3. Ombea tafsiri za Biblia katika lugha hizi kuu za eneo hili:: Khorasani Turkish, Afghan Sign Language, and Southwest Pashai.

**TUGEUKE KUTOKA KWENYE UBAGUZI TUUFIKIE UPENDO :**

Tumia muda makini kumwomba Bwana akuonyeshe watu ambao umekuwa na uchungu/kutokusamehe; nendeni kwao mwombe msamaha na umurudishiye unacho daiwa naye, ikibidi.

**PHILIPPIANS 2:3-4** *""Msifanye neno lo lote kwa kushindana, wala kwa majivuno; Bali, kwa unyenyekevu, kila mtu na amuhesabu mwenzake kuwa bora kuliko yeye mwenyewe, wala si kwa kuangalia faida zenu wenyewe bali kila mmoja wenu aingaliye faida ya wengine."*

# SIKU YA 5: KUGEUKA KUTOKA KWENYE KUBAKI TUMETULIA CHINI NA KUINGIA KWENYE HUDUMA

**WAFILIPI 2:5-8 "***Katika mahusiano yenu ninyi kwa ninyi iweni na nia moja kama Kristo Yesu aliyekuwa sawa na Mungu katika namna zote,  lakini hakufikiri kwamba kuwa sawa na Mungu kilikuwa kitu cha kungangania, badala yake, aliacha kila kitu hata sehemu yake pamoja na Mungu.Akakubali kuwa kama mtumwa,akiwa katika umbo la binadamu wakati wa maisha yake kama mtu,alijinyenyekeza na akawa mtiifu kabisa kwa Mungu, hata jambo hilo liliposababisha kifo chake msalabani.…"*

**KUABUDU :** Wewe ni MWOKOZI na MKOMBOZI[5]

> **ZABURI 18:16-19** *"Alipeleka kutoka juu akanishika; alinitoa katika maji mengi. Aliniokoa na adui yangu mwenye nguvu, na wale walionichukia, kwa maana walikuwa na nguvu kunishinda…"*
>
> **ISAYA 43:2** *"Upitapo katika maji mengi nitakuwa pamoja nawe; na upitapo katika mito, haitapita juu yako. Upitapo katika moto, hutateketea; mwali wa moto hautakuunguza."*

**KUTUBU (KUGEUZA NIA):** *Utusamehe kwa kung'ang'ania kubaki chini tumetulia, kwa ajili ya kuogopa kukufuata wakati tuonapo kuna hatari. Ututie ujasiri kwa upendo wako usiokwisha unaozima woga. Utusamehe dhambi zetu, Ee Mungu:*

- *Kuweka shughuli za kidini pahali pa kuwafikia na kuwaokoa waliopotea na wasiofikiwa bado na injili*
- *Shaka na kutoamini badala ya imani na utii*


**MITHALI 24:11-12** *"'Uwaokoe wale wanaopelekwa kwenye kifo; wazuie wale wanaojikongoja kuelekea machinjoni. Ukisema, "Lakini sisi hatukujuwa lolote kuhusu hili," je, yeye apimaye mioyo hatambui? Yeye anayelinda maisha yako hajui?"*

***Miji ingine ya Eneo hii :***

- Algiers, Algeria
- Tripoli, Libya
- Nouakchott, Mauritania
- Rabat and Marrakech, Morocco
- Muscat, Oman
- Dubai, UAE
- Tunis, Tunisia
- Sana'a, Yemen
- Mecca, Medina and Riyadh, Saudi Arabia
- Mosul, Basra, and Baghdad, Iraq
- Amman, Jordan
- Beirut, Lebanon
- Homs and Damascus, Syria
- Jerusalem, Israel

**KWA SAUTI KUBWA UWAALIKE WATU KUINGIA MAVUNONI HUKO: CAIRO, MISRI**

ENEO Moja Kati ya Miji 10: ***MASHARIKI YA KATI NA AFICA YA KASKAZINI (AFRIQUE DU NORD)***




*ENEO LOTE NZIMA : Lina Wakaaji milioni  402*
> *Hesabu ya Makabila ambayo bado hawana Kanisa hata moja kwenye miji yao : Makabila 398*
> *Hesabu ya Makabila ambayo kamwe hawaja fikiwa hata kidogo na Injili ni : Makabila 295*

**LUKA 24:46-47** *"Akawaambia, Ndivyo ilivyoandikwa, Masiya atateswa na kufufuka siku ya tatu, na toba na ondoleo la dhambi ziatahubiriwa kwa jina lake kwa mataifa yote, kuanzia. huko Yerusalemu."*

1. Waalike waamini wa Mungu kujitolea kukubali kupambana na hatari ikihitajika kwa ajili ya kuwatumikia wengine kwa upendo.
2. Ombea Mwili wa Kristo usogee kwa ujasiri kwenye maeneo ambapo bado Injili haija penya ili kuzalisha tena Ufalme wa Mungu hapo pia.
3. Ombea tafsiri za Biblia katika lugha hizi muhimu kwa eneo hili: Kisaanaani,  Kiharabu kinacho zungumuzwa Oman, & Lugha ya vidole ya huko Morocco .

**GEUKA KUTOKA KWENYE KUTULIA CHINI NA INGIA KWENYE HUDUMA:**
Ujitoleye siku ya leo kwa njia ya pekee kama dhabihu kwa kumtumikia mtu mwingine kwa njia ya vitendo, hasa asiyeamini. (Mf. Jitolea katika makao/benki ya chakula isiyo na makazi, tembelea makao ya wazee au wazee, n.k.)

**WARUMI 15:20-21**
*“Siku zote nia yangu imekuwa kuhubiri Injili mahali ambapo Kristo hakujulikana, nisije nikajenga juu ya msingi wa mtu mwingine. Badala yake, kama ilivyoandikwa: “Wale ambao hawakuambiwa habari zake wataona, na wale ambao hawajasikia wataelewa.”*

# SIKU YA 6: KUTOKA KWENYE HALI YA UCHUNGUZI TU KUFIKIA HALI YA KUJITOLEA KABISA-KABISA

***Miji mingine ya Eneo hili:***

- Djibouti, Djibouti
- Addis Ababa, Ethiopia
- Mombasa, Kenya
- Mogadishu, Somalia
- Khartoum, Sudan
- Dar es Salam, Tanzania

**2 NYAKATI 10:8** *“Sasa msiwe na shingo ngumu kama baba zenu; mkaingie patakatifu pake, alipotakasa milele, mkamtumikie BWANA, Mungu wenu, ili ukali wa ghadhabu yake usije ukawapata nyinyi.”*

**KUABUDU: Wewe ndiwe UNAYESTAHILI**[6]

> **JUDE 24-25** *“Kwake yeye awezaye kuwalinda ninyi msijikwae na kuwaleta ninyi mbele ya utukufu wake bila hatia na kwa furaha kuu — Mungu peke yake, aliye Mwokozi wetu, kwake uwepo utukufu, ukuu, nguvu na mamlaka kupitia Yesu Kristo kwa wakati uliopita, uliopo na milele. Amina..”*
>
> **UFUNUO 5:11-12** “*Kisha nikaona, nikasikia sauti ya malaika wengi, maelfu na elfu kumi mara elfu kumi. Wakakizunguka kile kiti cha enzi na wale viumbe hai na wale wazee. Walikuwa wakisema kwa sauti kuu: “Anastahili Mwana-Kondoo, aliyechinjwa, kupokea uwezo na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na sifa!”*


**KUTUBU (KUGEUZA NIA) :** *Utusamehe kwa kung’ang’ania kwetu ukaidi kwa ajili ya kuogopa, na kwa mashaka na kutoamini. Badala yake utusaidie kuacha kufuatana na mapenzi yetu bali tufuate mapenzi yako, Wewe uliye Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana. Utusamehe dhambi zetu, Ee Mungu;*

- *Ni Wewe tu, Bwana ndiye mwenye haki ya kutawala*
- *Kutii kwa moyo wote amri yako ndiyo huduma yetu nzuri ya kukuabudu Wewe Bwana*

**WARUMI 12:1-2** *“Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu ya kweli, inayostahili. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu...”*

**KWA SAUTI KUBWA UWAALIKE WATU KUINGIA MAVUNONI HUKO: DAR ES SALAM, TANZANIA**
Ni Eneo Moja kati ya Miji 10 : ***AFRIKA YA MASHARIKI & KUSINI***

*ENEO LOTE NZIMA : Lina Wakaaji milioni 621*
> *Hesabu ya Makabila ambayo bado hawana Kanisa hata moja kwenye miji yao : Makabila 355*
> *Hesabu ya Makabila ambayo kamwe hawaja fikiwa hata kidogo na Injili ni : Makabila 148*



**ZABURI 67:2** *"Ili njia yako ijulikane duniani, wokovu wako katika mataifa yote."*

1. Omba Mungu kwamba Roho amuwezeshe kila mwamini kumutegemea Yeye kabisa na kumtii Mungu kikamilifu katika kila jambo.
2. Ombea viongozi wa Mashirika ya Wavunaji waachiye Mungu Mwenyewe kazi ya kuzuia-zuiya wengine huku kila mumoja akiwa tayari kujitolea ku tembea kwenye Njia anazo zionyesha Roho wa Mungu
3. Ombea tafsiri za Biblia zifanyike katika lugha hizi kuu za Eneo hili : Hungu, Makhuwa-Saka, and Rombo.

**KUGEUKA KUTOKA KUZUIA-ZUIA ILI KUFIKIA KUJITOLEA KABISA KABISA:**

Mwombe Mungu akuonyeshe maeneo ya maisha yako ambayo unang'ang'ania kuyadhibiti. Tumia dakika 5 katika ukimya kumsikiliza Bwana. Andika kwenye karatasi maeneo unayohitaji kumwachilia Bwana, kisha, choma au pasua karatasi, hii ikiwa alama ya wewe kujiachilia. ("Make Room"; "Open Space")

**1 PETRO 4:1-2** *"Basi kwa kuwa Kristo aliteswa katika mwili kwa ajili yetu, ninyi nanyi jivikeni nia iyo hiyo; kwa maana yeye aliyeteswa katika mwili ameachana na dhambi, asipate kuishi tena wakati uliobakia katika mwili kwa tamaa za wanadamu, bali kwa mapenzi ya Mungu."*

***Miji mingine ya Eneo hili :***

- Ouagodougou, Burkina Faso
- N'Djamen'na, Chad
- Conakry, Guinea
- Bamako, Mali
- Niamey, Niger
- Nigeria: Ibadan, Kano, and Lagos
- Dakar, Senegal

# SIKU YA 7: KUACHA KUWAOGOPA WANADAMU NA KUANZA KUMUCHA MUNGU

**MITHALI 29:25** *"Kuwaogopa wanadamu huleta mtego; Bali amtumainiye BWANA atakuwa salama."*

**KUABUDU: Wewe unayo HAKI nayo KWELI**[7]

**ISAIAH 30:18** "*"Kwa hiyo Bwana anatamani kuwarehemu, na kwa hiyo anangoja juu ili awahurumie. Kwa kuwa Bwana ni Mungu wa haki; Wamebarikiwa sana wale wote wanaomtamani."*

> **UFUNUO WA YOHANA 15:2-4** *"Na nikaona kitu kama bahari ya kioo imechanganyika na moto. Na kando ya hiyo bahari, walikuwa wamesimama wale watu waliom shinda yule mnyama na sanamu yake pamoja na namba ya jina lake. Walikuwa wameshika vinubi walivyopewa na Mungu. 3 Nao waliimba wimbo wa Musa, mtumishi wa Mungu na wimbo wa Mwana-Kondoo wakisema, ' 'Matendo yako Bwana Mungu Mwenyezi, ni makuu na ya ajabu! Njia zako wewe Mfalme wa Mataifa ni za haki na za kweli! 4 Ni nani asiyekucha wewe Bwana na kulitukuza jina lako? Kwa kuwa wewe peke yako ni mtakatifu. Mataifa yote yatakuja na kukuabudu kwa kuwa matendo yako ya haki yamekwisha dhihirishwa.""*

**KUTUBU (KUGEUZA NIA):** *Utusamehe kwa kujali zaidi maoni ya wengine kuliko Yako. Usogeze mioyo yetu kujitoa kikamilifu Kwako kwa uaminifu kamili. Utusamehe dhambi zetu, Ee Mungu :*

- *Ibada ya sanamu ya kupenda vitu au watu wengine zaidi yako*
- *Kuwa mtumwa wa hofu badala ya kutembea katika uhuru wa Bwana*

**ISAYA 33:6** *"Naye Bwana atakuwa ndiye utulivu wa nyakati zako, wingi wa wokovu, na hekima na maarifa; Kumcha Bwana ni hazina yake."*

**KWA SAUTI KUBWA UWAALIKE WATU KUINGIA MAVUNONI HUKO: LAGOS, NIGERIA**
Ni Moja kati ya Miji 10 : ***AFRIKA YA KATI NA YA MAGARIBI***




***Miji ingine ya Eneo hii:***

- Uturuki: Ankara, Gaziantep, Diyarbakir, Antalya, and Istanbul
- Kazan and Moscow, Russia
- Athena, Ugiriki (Grece)
- Paris, Ufaransa (France)
- London, United Kingdom

*ENEO LOTE NZIMA : Lina Wakaaji milioni 587.5*

*Hesabu ya Makabila ambayo bado hawana Kanisa hata moja kwenye miji yao : Makabila 459*

*Hesabu ya Makabila ambayo kamwe hawaja fikiwa hata kidogo na Injili ni : Makabila 180*

**MATAYO 24:14** *"Injili hii ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; hapo ndipo ule mwisho utakapokuja."*

1. Ombea waamini wampendeze na kumtii Mungu kuliko wanadamu.
2. Ombea wafanya wanafunzi kuangusha sanamu zozote na kumfuata Mungu peke Yake.
3. Ombea tafsiri za Biblia katika lugha hizi muhimu kwa eneo hili: region: Wasa, Nago ya Kusini, and Ayizo Gbe.

**GEUKA KUTOKA KUOGOPA MWANADAMU UPATE KUMCHA MUNGU :**
Elezea hadithi yako (ushuhuda) wa uaminifu wa Mungu na msamaha kwa mtu mpya leo.

**ZABURI 128:1-4** *"Heri wote wamchao Bwana, waendao katika kumtii. Utakula matunda ya kazi yako; baraka na mafanikio yatakuwa yako. Mkeo atakuwa kama mzabibu uzaao ndani ya nyumba yako; watoto wako watakuwa kama mizeituni kuzunguka meza yako. Naam, hii itakuwa baraka kwa mtu anayemcha Bwana."*

# SIKU YA 8: KUACHA MOYO WA CHOYO NA KUGEUKA MTU WA UKARIMU

**MITHALI 11:24** *"Mtu mmoja hutoa bure, lakini hupata zaidi; mwingine hunyima isivyostahili, bali huwa maskini."*

**KUABUDU: Wewe ni MUKARIMU SANA**[8]

> **WARUMI 8:31-32** *"Tuseme nini basi katika mambo haya? Ikiwa Mungu yuko upande wetu, ni nani aliye juu yetu? Yeye asiyemwachilia Mwana wake mwenyewe, bali alimtoa kwa ajili yetu sisi sote, atakosaje kutukirimia na mambo yote pamoja naye?"*
>
> **2 PETRO 1:3** *"Uweza wake wa Uungu umetukirimia kila kitu tunachohitaji ili tuishi maisha ya utauwa kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe."*

**KUTUBU (KUGEUZA NIA) :** *Utusamehe kwa kung'ang'ania kwa ubinafsi mali zetu duni badala ya kuiga ukarimu wako wa hali ya juu na kutoa bure, tukijua Utatupatia kila tunachohitaji tunapokutafuta Wewe kwanza. Utusamehe dhambi zetu, Ee Mungu;*


---

- *Uchoyo tunao onyesha katika kuyumia wakati wetu, vitu vyetu vya bei gali, na vipaji tulivyo navyo*
- *Kutokushukuru kwa mambo mbalimbali aliotunyeshea kwa uwingi*




**MATAYO 6:33** *“"Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote* mtazidishiwa."

**KWA SAUTI KUBWA UWAALIKE WATU KUINGIA MAVUNONI HUKO: MOSKO, URUSSI** NI ENEO MOJA KATI YA MIJI 10 : ***ULAYA / ENEO LA KATI YA ULAYA NA ASIA***




*ENEO LOTE NZIMA : Lina Wakaaji milioni 746*
*Hesabu ya Makabila ambayo bado hawana Kanisa hata moja kwenye miji yao : Makabila 574*
*Hesabu ya Makabila ambayo kamwe hawaja fikiwa hata kidogo na Injili ni : Makabila 260*

**ZABURI 86:9** *“Mataifa yote uliyoyafanya yatakuja na kusujudu mbele zako, Ee Bwana; watalileta utukufu jina lako.”*

1. Ombea waamini kuondokana na mfumo wa ulimwengu wa kununua na kuuza wa ingiye katika utoaji na kupokea kupitia Ufalme wa Mungu.
2. Ombea Mwili wa Kristo kuwafikia kwa ukarimu wanadiaspora na wakimbizi katika eneo hili.
3. Omba kwa ajili ya tafsiri ya Biblia katika lugha hizi katika eneo hili: Pontic Greek, Montenegrin, na ki Romano-Serbian.

**KUACHA MOYO WA CHOYO NA KUCHUKUWA MOYO WA UKARIMU:**

Leo, unda zawadi au chakula cha kujitengenezea nyumbani na umpe jirani au mtu ambaye kwa kawaida hungeli mupa zawadi hii , au toa zawadi ya pesa bila kujulikana.

**2 WAKORINTO 9:10** “Na Mungu anaweza kuwapa kila baraka kwa wingi wa kushangaza, ili kila wakati muwe na kila kitu kwa kiasi cha kutosha na ziada kwa ajili ya kila kazi njema. [9] Kama Maandiko yanavyosema, “Yeye hutapanya kila mahali kuwapa maskini, haki yake hudumu milele. *Mungu huyu mkarimu zaidi anayempa mkulima mbegu ambayo inakuwa mkate kwa milo yenu ni zaidi ya fujo nanyi. Anawapa kitu ambacho mnaweza kutoa, ambacho kinakua hadi kufikia ukamilifu wa uzima, imara katika Mungu, mkiwa na utajiri wa kila namna, ili mpate kuwa wakarimu katika kila jambo, mkimtolea Mungu sifa kuu pamoja nasi.”*

# SIKU YA 9: KUACHA KUISHI KWA AJILI YA MAMBO YA ULIMWENGU NA KUANZA KUISHI KWA AJILI YA UFALME WA MUNGU

**WAGALATIA 5:16-18** *“Nasema, mruhusuni Roho atawale maisha yenu na msitafute kutimiza tamaa za mwili. 17 Kwa maana tamaa za mwili hushindana na Roho; na Roho hushindana na tamaa za mwili. Roho na mwili hupingana, na kwa sababu hiyo ninyi hamwezi kufanya yale mnayotaka. 18 Lakini kama mkiongozwa na Roho, hamko tena chini ya sheria.*

*.”*

**KUABUDU: Wewe ndiwe TUZO**[9]

**WAFILIPI 3:7-13** *" Lakini mambo hayo niliyoyaona mwanzo kuwa ni faida kwangu, sasa nayaona kuwa ni hasara kwa ajili ya Kristo. 8 Zaidi ya hayo, nahesabu mambo yote kuwa hasara tupu yakilinganishwa na faida kubwa ninayopata kwa kumjua Kristo Yesu aliye Bwana wangu. Kwa ajili yake nilikubali kupoteza kila kitu na kuona mambo hayo yote kuwa ni takataka ili nipate faida ya kuwa na Kristo; 9 na nikiwa kwake nisionekane kama mtu mwenye haki yake mwenyewe, inayotokana na kushika sheria, bali niwe na ile haki inayotokana na kumwamini Kristo, ambaye yeye ni haki itokayo kwa Mungu inayopatikana kwa imani. 10 Nataka nimjue Kristo na nguvu ya ufufuo wake na nishi riki mateso yake, niwe kama yeye katika kifo chake; 11 na hivyo, kama ikiwezekana, niufikie ufufuo kutoka kwa wafu. 12 Sisemi kwamba nimekwisha kupokea haya yote, au kwamba nimekwisha kuwa mkamilifu, la hasha; bali nazidi kukaza mwendo ili nipate kile ambacho, kwa ajili yake, Kristo amenifanya niwe wake. 13 Ndugu zangu, bado sijihesabu kuwa nimekwisha pata ile zawadi. Lakini jambo moja ninalofanya ni kusahau mambo yote yali yopita, na kukaza mwendo kufikia yaliyo mbele yangu.*

***Miji ingine katika hii Eneo:***

- Mexico City, Mexico
- Sao Paolo, Brazil
- Buenos Aires, Argentina
- Lima, Peru
- Santiago, Chile
- Havana, Cuba

**KUTUBU (KUGEUZA NIA) :** *Utusamehe kwa kutulia katika mambo madogo madogo ya ulimwengu huu badala ya kukufuata Wewe uliye Hazina ya Kweli na utawala wako wa haki. Utusamehe dhambi zetu, Ee Mungu;*

- *Kufuatia na kuridhika na mambo ya papo hapo badala ya thawabu ya milele*
- *Uvivu na kuanguka badala ya uvumilivu wa kudumu*




**2 WAKORINTO 4:17-18** "*Mateso yetu ni mepesi na ya muda tu na yanatuletea utukufu wa milele ambao ni mkuu kuliko chochote tunachoweza kufikiria. Hatutafuti vitu vinavyoonekana bali vitu visivyoonekana. Mambo yanayoonekana ni ya muda tu, lakini yasiyoonekana ni ya milele.forever."*

**KWA SAUTI KUBWA UWAALIKE WATU KUINGIA MAVUNONI HUKO : SAO PAULO, BRAZIL**

*ENEO LOTE NZIMA LA LATIN AMERIKA : Lina Wakaaji milioni 613.9*
*Hesabu ya Makabila ambayo bado hawana Kanisa hata moja kwenye miji yao : Makabila 104*
*Hesabu ya Makabila ambayo kamwe hawaja fikiwa hata kidogo na Injili ni : Makabila 53*

**ZABURI 96:3** *"Tangazeni utukufu Wake kati ya mataifa, Na watu wote habari za ajabu Zake."*

1. Ombea waamini wapate ufunuo kuhusu jinsi oyo wa Mungu unavyo hisi kuhusu walio dhambini na wale ambao hawajafikiwa bado na Injili na pia Chukuwa hatua ya luwaendea kwenye shamba la mavuno.
2. Omba kwa ajili ya makanisa iweze kuwa sapoti watendakazi walio watuma na waache kubakia wametulia bali wageuke kuwa Wanafunzi wa Yesu wanai fanya wengine kuwa pia Wanafunzi wa Yesu.
3. Ombea tafsiri za Biblia katika lugha hizi muhimu kwa eneo hii : Embera-Baudo, Puebla na Northeastern Mazatec, na Tepinapa Chinantec.

**GEUKA KUTOKA KUISHI KWA AJILI YA ULIMWENGU ILI KUISHI KWA AJILI YA UFALME WA MUNGU:**

Pitia simu/kompyuta yako na ufute/uondoe vikengeushi vinavyochukua muda lakini ambavyo havijazingatia mambo ya Ufalme wa Mungu. (Mf. Michezo ya Simu Mahiri, Mitandao ya Kijamii, DVD, n.k.)

**WAEBRANIA 6:10-11** "*Mungu si dhalimu; hataisahau kazi yenu na upendo mliomwonyesha…"*
*"*

# SIKU YA 10: KUACHA KUTAZAMA NYUMA NA KUANZA KUTAZAMA JUU

**LUKA 21:28** *"Basi mambo hayo yaanzapo kutokea, simameni, mkaviinue vichwa vyenu, kwa maana ukombozi wenu umekaribia".*

**KUABUDU : Wewe ndiye NYOTA INAYONG'AA ASUBUHI**[10]

> **UFUNUO 22:16-17** *"Mimi, Yesu, nimemtuma malaika wangu kuwatolea ninyi ushuhuda huu kwa ajili ya makanisa. Mimi ndimi niliye Shina na Mzao wa Daudi, na ile Nyota ya Asubuhi yenye kung'aa." Roho na bibi-arusi wanasema, "Njoo!" Na yule anayesikia na aseme, "Njoo!" Mwenye kiu na aje; naye anayetaka na ayatwae maji ya uzima bure."*

***Miji ingine katika hii Eneo :***

- USA: New York City, Los Angeles, Dallas / Ft. Worth, and Miami.
- Toronto, Canada


**KUTUBU (KUGEUZA NIA) :** *Utusamehe kwa kulemewa na masumbuko na kufungwa katika dhambi zetu. Utukumbushe kuinua macho yetu kwa kutarajia ujio wako na kushughulika kikamilifu hadi Utakapotokea. Utusamehe, Ee Mungu:*

- *Masumbuko ya ulimwengu huu na udanganyifu wa mali*
- *Mambo madogo yanayozuia mambo ya maana zaidi*

**WAEBRANIA 12:1** *"Basi, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile inayotuzinga kwa ukaribu; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu …"*

**KWA SAUTI KUBWA UWAALIKE WATU KUINGIA MAVUNONI HUKO: Muji wa NEW YORK CITY, NEW YORK, MAREKANI**

*ENEO LOTE NZIMA LA LATIN AMERIKA : Lina Wakaaji milioni 420.3*
*Hesabu ya Makabila ambayo bado hawana Kanisa hata moja kwenye miji yao : Makabila 168*
*Hesabu ya Makabila ambayo kamwe hawaja fikiwa hata kidogo na Injili ni : Makabila 57*




**WAFILIPI 2:10-11** *"ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba.."*

1. Ombea waamini waanze kuokoa wakati, wakijaza taa zao na mafuta katika maandalizi ya kurudi kwa Yesu Kristo katika utukufu.
2. Ombea kanisa liwe likiishi na kufanya kazi katika kutarajia kurudi kwa Yesu hivi karibuni.

3. Ombea Tafsiri za Biblia katika lugha hizi muhimu: Kiingereza, Bahamas na Creole, Creole ya Kiingereza ya Grenadi, na Creole ya Kituruki na Caicos Kiingereza (Bahamas English Creole, Grenadian English Creole, and Turks and Caicos English Creole).

**GEUKA KUTOKA KUANGALIA NYUMA ILI KUTAZAMA JUU:**

Kaza macho yako juu ukingojea kurudi kwa Kristo. Zungumza na watu munao ishi nao walio waamini kuhusu jinsi munavyoweza kujaza taa zenu mafuta kwa bidii na kuwa tayari kwa ajili ya kurudi kwa Yesu Kristo Mfalme wetu wa Bwana wa mabwana.

**2 TIMOTHY 4:8** *"Basi nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana, mhukumu mwadilifu, atanikabidhi siku ile; wala si mimi tu, bali na wote waliotamani kufunuliwa kwake*. ."

**NINI KITAFUATA?** Weka maombi yako kwenye vitendo.

*Kundi la SIKU 10 ZA MAOMBI NA KUFUNGA ina furaha kushirikiana na BigLife ili kukusaidia kuchukua hatua inayofuata katika kutii amri ya Yesu. "Biglife inawawezesha waamini ulimwenguni kote kufikia na kuwafunza watu wanao ishi nao wenyewe kwa ajili ya Yesu, ili mienendo ya Mungu ya kufanya wanafunzi iweze kukomaa na kuongezeka duniani kote."*

Pata mafasiriyo ya kuongezea: https://big.life or www.10days.net/dmm-training

**JE, UNATAKA KUENDELEA KUOMBA PAMOJA NA WENGINE ULIMWENGUNI?**

[1] Ombea Miji 110 & Ambayo Haijafikiwa Kila Wiki kwa kutumia Funguo za Wanafunzi.

Jifunze Zaidi: https://www.disciplekeys.world/disciplekeys-pray/

[2] Jiandikishe ili Kuanza tabia ya Kuombea mji mmoja kwa kuchukuwa dakika 15 kila siku, au kila wiki kwa ajili ya kuziombea shuguli za injili katika miji 110 ambayo haijafikiwa ulimwenguni. Asilimia 98 ya watu waliosalia ambao hawajafikiwa na injili wanawakilishwa katika majiji haya.
Jifunze Zaidi: : http://110cities.pray4movement.org

[3] Njoo tuombe pamoja na Global Family 24/7 Maombi ya Mtandaoni.

*10 Days 2020 left many feeling hungry for more intercession with others around the world. This led to the birthing of the 24/7 Online Prayer Room that hosts leaders from over 50 nations praying in more than 25 languages around the clock since January 1st, 2021. We would love to have you join us in prayer through Global Family.*

*Tulipo omba kipindi cha Siku 10 katika mwaka wa 2020, watu wengi walibaki wakihisi njaa ya maombezi zaidi na wengine kote ulimwenguni. Hili lilipelekea kuanzishwa kwa Chumba cha Maombi ya Mtandaoni cha 24/7 ambacho hukaribisha viongozi kutoka zaidi ya mataifa 50 wakiomba katika zaidi ya lugha 25 kila saa tangu Januari 1, 2021. Tungependa ujiunge nasi katika maombi kupitia Global Family.*

Pata habari zaidi hapa: linktr.ee/globalfamily247

**WASHIRIKA:**

Asante kwa ndugu na dada wenzetu katika Kristo ulimwenguni kote ambao wametangaza jina la Yesu kote ulimwenguni siku hizi 10 zilizopita!

Global Family 24/7 Prayer, Aqueduct Project, Come to the Table, International Prayer Connect, 110Cities, Big.Life, Run Ministries, 24:14, The Return, Billion Soul Harvest, Pray for Zero, Go Movement, Reconnecting Ministries, Fellowship of Prayer Strategists, Disciple Keys, and Ethnê Prayer Movement.